

3.2 KISWAHILI (102)

3.2.1 Kiswahili Paper (102/1)

1. Lazima

Wewe ni katibu wa jopokazi ambalo limeteuliwa kuchunguza sababu za wanafunzi wa shule za upili kupuuza masomo ya kiufundi. Andika ripoti ya uchunguzi huo huku ukitoa mapendekezo.

2. Maktaba ya shule yenu haina magazeti. Andika makala kuonyesha umuhimu wa maktaba hiyo kuwa na magazeti.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Mpanda ovyo hula ovyo.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:

Msongamano wa wanunuzi, wapitanjia na wasukuma mkokoteni katikati mwa wachuuzi wa kila aina ulinitanabahisha kuwa nimefika mji wa Tifaruku.